SEHEMU YA III – WAKATI WA MUNGU

Wakati katika Uwepo wa Bwana Mtakatifu kwa Kuabudu na Kuomba

Kuvaa Silaha Zote za Mungu

Fanya ombi hili liwe sehemu ya shughuli zako zote za asubuhi. Hili ombi litakusaidia kujiandaa kukabiliana na changamoto zote za kiroho katika nguvu na uwezo wa Mungu.

Bwana mpendwa, ninapotoka kitandani leo, ninajua ninaondoka kwenda kwenye uwanja wa vita. Ninajua pia kwamba umenipa kila kitu ambacho ninahitaji ili kusimama imara. Kwa hivyo, kwa nguvu za roho mtakatifu ninavaa silaha zote za Mungu.

Kwanza, ninaiweka chepeo ya wokovu kwenye kichwa changu. Naomba ukakinge nia zangu na mawazo yangu. Naomba ukayalinde macho yangu na kuzuilia dhambi yoyote isiniingie. Tafadhali yatilie mkazo macho yangu kwa mambo ya Mungu. Acha dirii ya haki ilinde na iweke moyo wangu na hisia zangu salama. Naomba ya kwamba sitaongozwa na jinsi ninavyojisikia bali nitaongozwa na ukweli. Ninajizungusha na neno lako kama mshipi. Tafadhali unilinde na makosa yoyote yale. Ninavaa viatu vya amani viongoze hatua ya miguu yangu. Tafadhali panda miguu yangu kwa ukeli wako. Nipe uwezo wa kusimama imara kinyume cha mashambulizi.

Kisha, ninatwaa ngao ya imani. Bwana naomba unilinde na mishale ya moto ya shetani. Niweke bega kwa began na jeshi lako ili kuja kinyume na hila zote za shetani. Mwishowe, ninatwaa upanga wa roho, ambao ni neno lako takatifu, Bwana. Naomba unisaidie kusoma neno lako kwa njia mpya za kusisimua ili niweze kupinga mashambulizi na kushiriki ukweli wa neno lako na wengine.

Ninajua nitakumbana na mashambulizi siku ya leo, Bwana lakini umenitia nguvu kuweza kusimama imara. Bwana, naomba unipe nguvu kwa ajili ya vita leo. Furaha ya Bwana ni nguvu zangu. Kwa jina la Yesu, nimeomba. Amina.

Maandiko ya kurejelea (Waefeso 6:13-18)

Sala ya Bwana

Baba yetu uliye mbinguni

Jina lako litukuzwe

Ufalme wako uje

Mapenzi yako yatimizwe

Hapa duniani kama huko mbinguni

Utupe leo riziki yetu

Utusamehe makosa yetu
Jinsi tunavyowasamehe waliotukosea
Na usitutie majaribuni
Lakini utuokoe na ule mwovu
Kwa kuwa ufalme ni wako
Na nguvu na utukufu hata milele
Amina

Maandiko ya kurejelea (Matthew 6: 9-13)

<u>Maombi ya Ulinzi wa Bwana</u>

Sisi, tunaoketi mahali pa siri pake Aliye juu
Tutakaa katika uvuli wake Mwenyezi.
Nitasema kwake Bwana " Wewe ndiwe kimbilio langu na ngome yangu;
Mungu wangu nitakayemtumaini.

Kwa hakika utakuokoa na mtego wa mwindaji
Na katika tauni iharibuyo.
Utatufunika kwa manyoya yako,
Chini ya mbawa zake tutapata kimbilio;
Uaminifu wako utakuwa ni ngao na kigao.
Hatutaogopa hofu ya usiku, wala mshale urukao mchana,
Wala tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri,
Ijapo watu elfu waanguka ubavuni mwetu,
Naam, kumi elfu mkono wetu wa kuume
Hata hivyo haitatukaribia sisi
Ila kwa macho yetu tutatazama,
Na kuyaona malipo ya wasio haki.

Kwa kuwa tumekufanya wewe Bwana, ndiwe kimbilio letu
Hata Aliye juu kuwa makao yetu,
Mabaya yoyote hayatatupata sisi,
Wala tauni haitaikaribia hema yetu
Kwa kuwa utakuagizia malaika wako watulinde katika njia zetu zote
Mikononi mwao watatuchukua,
Tusije tukajikwaa miguu katika jiwe.
Tutawakanyaga simba na nyoka,
Mwana-simba na joka tutawakanyaga kwa miguu.

“ Kwa kuwa tumekaza kukupenda, kwa hivyo utatuokoa;
Utatuweka palipo juu, Kwa kuwa tumelijuajua Jina lako.
Tutakuita nawe utaitika;
Utakuwa pamoja nasi taabuni,
Utatuokoa na kututukuza;
Kwa siku nyingi utatushibisha,
Na kutuonyesha wokovu wako.”

Maandiko ya kurejelea (Zaburi 91)

Bwana Ndiye Mpeanaji Wetu (Anashughulikia Mahitaji Yetu Yote)

Bwana, wewe ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu. Nina kila kitu ninachohitaji
Unanilaza katika malisho ya majani mabichi,
Unaniongoza kando ya maji ya utulivu,
Unanihuisha nafsi yangu; Unanipa nguvu mpya
Unaniongoza katika njia za haki ukileta utukufu kwa jina lako.
Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa ,
Kwa maana wewe Bwana upo pamoja nami,
Gongo lako na fimbo yako vyanifariji.
Unaandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu.
Umenipaka mafuta kichwani pangu,
Na kikombe changu kinafurika kwa baraka
Kwa hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu;
Na Bwana, nitakaa nyumbani mwako milele.

Maandiko ya Kurejelea (Zaburi 23)

Maombi ya Saa Tisa

Yesu ulikufa, lakini chanzo cha maisha kikabubujika kutuka kwako kwa ajili ya nafsi
Na bahari ya rehema ikafunguka kwa ajili ya ulimwengu wote
Ewe chemchemi ya uzima, rehema zakiungu zisizoeleweka
Kumbatia ulimwengu wote na ukajimwage kwetu
Damu na maji
Iliyotiririka kutoka kwa moyo wa Yesu
Kama chemchemi ya rehema kwa ajili yetu
Tunakuamini wewe
Mungu mtakatifu, Mtakatifu mwenyezi, Mtakatifu uishiye milele

Uturehemu sisi pamoja na ulimwengu wote kwa ujumla
Yesu Kristo mfalme, mfalme wa rehema, tunakuamini wewe. Amina

Kutafuta Uongozi wa Mungu

Bwana, ninatafuta uongozi wako kwa ajili ya maamuzi ninayotakiwa kufanya. Ninatafuta mapenzi yako kwa ajili ya maisha yangu. Bwana, ninakuamini kwa moyo wangu wote. Sitegemei ufahamu wangu. Ninatafuta mapenzi yako kwa ajili ya yote niyatendayo. Na Bwana, ninajua ya kwamba utanionyesha njia ya kufwata.

Bwana, naomba unifundishe kutulia katika uwepo wako mtakatifu. Nifunze niweze kusikia sauti yako tulivu. Nibariki ili niweze kukutii na kufwata maagizo yako. Bwana, acha iwe kwangu kulingana na neno lako na mapenzi yako.

Baba, katika jina la Yesu, naomba. Amina.

Maandiko ya kurejelea (Mhubiri 3: 5 - 6)

Ombi la kushinda kusumbuka, kukosa utulivu na wasiwasi

Mungu mwenyezi, naja kwako kwa maombi. Unajua yale ninayopitia. Nina wasiwasi na ninakosa utulivu. Bwana, ninajua ya kwamba haisaidii chocote nikiwa na wasiwasi na kusumbuka. Ninajua wewe ni Mungu mwenyezi, mwenye nguvu na mwenye upendo. Naja kwako nikitafuta Baraka zako na amani yako. Ninajua kwamba unaalika watoto wako wote waje kwenye uwepo wako, pamoja na wale walio kama mimi, waliochoka na kulemewa na mizigo mizito. Na ninajua kwamba umeniahidi pumziko ndani yako.

Bwana, ninapeana wasiwasi na masumbuko yangu yote kwako kwa sababu unanijali. Ahsante, Bwana. Wewe ni mtulivu na mnyenyekevu wa moyo. Nitapata pumziko ndani yako. Ninainua pia kwa maombi watoto wako wapendwa katika ulimwengu huu wanaopitia hali kama zangu. Tubariki na amani yako.

Baba, ninauliza haya kwa maombi kwa jina kuu la Yesu. Amina

Maandiko ya kurejelea (Mathayo 11: 28-30, Waraka wa Kwanza wa Petro 5:7)

Maombi ya Uponyaji

Mungu mwenyezi, wewe ni mtakatifu na mwenye haki Una nguvu na rehema. Mamlaka yote mbinguni na kwenye ardhi ni yako.

Mungu mwenye upendo, wewe ni Mungu wa neema. Umetupatia sisi sote uzima, Wewe ni mwokozi. Mikononi mwako na mamlakani mwako, kuna nguvu ya uponyaji dhidi ya magonjwa na wasiwasi.

Jinsi gani ulivyo na upendo na rehema. Ulitupatia mwana wako mpendwa, Yesu Kristo mkombozi wetu. Dhambi zetu zote na magonjwa yetu yote yalioshwa kwa mapigo ya uponyaji ya Yesu na damu yake takatifu. Tumepona!

Ninakiri udhaifu wangu wote na dhambi zangu zote. Nisamehe, Bwana. Mimi ni kitu bure bila wewe na ni kwa neema yako tu nimepona. Wewe ni Mungu wa miujiza. Ninaamini katika nguvu za ukuu, upendo na rehema zako. Umenisamehe na kuniponya. Bwana, ninakushukuru kwa kunipa moyo mpya na msafi. Bwana nakushukuru kwa kunipa amani yako. Naomba uwe nami daima. Wewe ni Imanueli (Mungu yu nasi).

Wewe ni njia, ukweli na uzima. Wewe ni nuru ya maisha yangu. Nimeokoka na upendo wako kwangu. Nifunike kwa damu yako ya thamani na takatifu, ewe Bwana.

Nivute karibu nawe, Bwana Yesu. Naamini katika nguvu zako kuu. Wewe ni mwokozi, mponyaji, mlinzi na maficho. Wewe ni Mungu wangu.

Bwana Yesu, unajua kila kitu kunihusu, mahitaji yangu na matamanio yangu. Kwa mikono yako mikuu na mitakatifu, ninajikabidhi. Wacha iwe kwangu kulingana na mapenzi yako. Mimi ni wako. Nimeokoka na kupona.

Baba, naomba vilevile kwa ajili ya kaka na dada zangu wanaohitaji neema na Baraka. Ninauliza maombi haya kwa jina kuu la Yesu Kristo. Amina

Maandiko ya Kurejelea (Isaya 53:5, Zaburi 103: 1-5, Yohana 14:6)

Kutupa Mbali Mawazo Mabaya Na Mienendo Mibaya kwa Nguvu na Mamlaka ya Mungu

Bwana mpendwa, najua Baraka zako na neema zako ziko juu yangu. Ninang'ang'ana na mawazo mabaya na mienendo mibaya ambayo haistahili machoni pako. Ninataka kutupa mbali haya mawazo mabaya na mienendo mibaya. Ninakushukuru kwa kunipa nguvu na mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge, na juu ya nguvu zote za adui, na hakuna jambo lolote litanidhuru.

Kwa hivyo, katika jina kuu la Yesu, ninaamuru haya mawazo mabaya na mienendo kuniacha sasa hivi. Bwana, naomba unioshe kwa damu yako ya thamani na unitakase kutokana na dhambi hizi. Nijaze na neema na huruma zako. Acha nikaishi kuliinua na kulitukuza jina lako takatifu. Ninaomba katika jina kuu la Yesu. Amina.

Maandiko ya Kurejelea (Luka 10: 19)

Maombi ya Amani

Bwana, moyo wangu unasumbuka. Sina amani. Ninajaribu kuzuia nia zangu lakini mawazo ya kusumbua yanazidi kuja. Bwana Yesu, umeahidi amani kwa watoto wako. Ulisema kwamba , “Amani ninawaachieni, amani yangu nawapa; siyo jinsi dunia inavyowapa. Msiache mioyo yenu kusumbuka, na wala msiogope”.

Bwana Yesu, ninaamini ahadi zako. Ninakuamini. Ahsante Bwana, kwa kuwepo kwa ajili yangu. Nalisifu jina lako. Ninakabidhi wasiwasi zangu kwako kwa maana unanijali. Na ninaamini ya kwamba amani yako iko juu yangu. Amani yako inafanya kazi ndani yangu. Amani yako inapita ufahamu wowote wa mwanadamu. Ahsante Bwana.

Bwana, ninajua utawaweka kwa amani kamilifu wale wote wanakuamini wewe na wale wote mawazo yao yako juu yako. Ninakuamini, Bwana. Wewe ndiwe mwamba wa milele na nguvu zetu zinazodumu milele. Nitalala chini kwa amani na nilale, kwa kuwa ni wewe pekee, Bwana ambaye ataniweka salama.

Ninawaombea pia watoto wako ambao hawana amani ndani ya mioyo yao. Acha amani yako ikaweze kugusa mioyo yao na kuwafariji. Baba ninauliza hili ombi kwa jina kuu la Yesu. Amina

Maandiko ya Kurejelea (Yohana 14: 27, Zaburi 4:8, Isaya 26: 3-4, Petero wa Kwanza 5:7, Wafilipi 4: 6-7)

Maombi ya Kuomba Msamaha kwa Makosa Yangu na Dhambi Zangu`

Baba mpenzi uishiye mbinguni, niruhusu nije kwenye uwepo wako mtakatifu na nikae miguuni pako. Ninatafuta msamaha wako kwa dhambi zote nimetenda katika mawazo yangu, usemi wangu na matendo yangu.

[[[Omba msamaha kwa dhambi zote na makosa yote uliyotenda:

- *Utotoni mwako*
- *Kama kijana*
- *Mahali pako pa kazi/ shuleni*
- *Katika mahusiano yako na watu wa jamii yako*
- *Katika mahusiano yako na watu wa jamii yako na marafiki*
- *Katika mahusiano yako na watu wengine*

Leta kwa Bwana makosa yote ambayo umewahi kufanya na umuombe msamaha]]]

Bwana, ninawezaje kujua dhambi zote ambazo zimejificha moyoni mwangu? Ni nani awezaye kupambanua makosa yake mwenyewe? Naomba usamehe makosa yangu yaliyofichika. Nisafishe kutokana na makosa haya yaliyofichika. Niweke mbali na makosa yatendwayo kimaksudi. Usiyaache yanitawale. Ndipo nitakuwa huru kutokana na hatia na kutokuwa na hatia ya dhambi kuu.

Nimetenda dhambi na ni kwa neema yako tu, ndiposa dhambi zangu zimeoshwa kwa sababu nakubali Yesu Kristo in mwokozi wangu. Alikuja ulimwenguni kuchukua dhambi zangu na magonjwa yangu. Ni kwa neema yake na kwa kifo chake msalabani kwa ajili yetu, ndiposa ninaweza kukuita baba yangu.

Bwana, wewe ni mwenye nguvu na mwenye upendo. Uliokoa mji wa Nineveh na ukawakomboa watu wote huko walipotubu dhambi zao. Bwana, wewe ni Mungu mwenye neema na huruma, mwepesi wa hasira na mwingi wa upendo na fadhili.

Naomba unitakase na uoshe moyo wangu na nia yangu. Unisamehe dhambi zote nilizotenda. Nioshe kwa damu ya thamani ya yesu na unitakase. Ninakushukuru na kulisifu jina lako kuu na takatifu

Acha maneno ya midomo yangu na kutafakari kwa moyo wangu kukubalike machoni pako. Ewe Bwana, wewe ni nguvu zangu na mkombozi wangu. Naomba unisamehe na unibariki na amani yako, upendo na furaha. Naomba uibariki jamii yangu pia.

Baba, nimeomba katika jina kuu na takatifu la Yesu Kristo. Amina.

Maandiko ya Kurejelea (Zaburi 19: 12-14)

Maombi ya Kutuwezesha Kuwasamehe Wengine

Baba mpenzi wa mbinguni, mimi nimeumia. Ninajisikia kuwa sitaweza kusamehe *[[[taja jina la Yule mtu ambaye unaona ugumu kusamehe]]].* Ninapata ugumu kusahau kisa hiki kilichotokea. Lakini Bwana, ninajua hutaki nibebe hali ya kutosamehe moyoni mwangu. Kuna mengi sana ninaweza kujifunza kutoka kwako. Ulimtuma mwanao wa pekee, Bwana wety Yesu Kristo hapa ulimwenguni kunifilia pale msalabani na kuchukua dhambi zangu zote na magonjwa yangu. Katika damu yake ya thamani, dhambi zangu zimesamehewa na kuoshwa milele. Na Baba, umesema kwamba hutakumbuka dhambi zangu za kale tena.

Bwana, nifunze kuwa mwema na kuwaonea wengine huruma. Nifundishe kuwasamehe wengine, jinsi ulivyonisamehe mimi kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Baba, ninaomba kwa jina kuu la Yesu. Amina

Maandiko ya Kurejelea (Waefeso 4:32, Waebrania 10: 17)

Maombi ya Kushinda Woga

Baba mpendwa uishiye mbinguni, jina lako takatifu ni ngome imara. Ninakukimbilia na ninakuwa salama. Wewe ni Bwana wangu na Mungu wangu. Wewe ni Emanueli, Mungu pamoja nasi. Yule aliye ndani yangu ni mkuu kulikob Yule aliye duniani. Mimi sitaogopa.

Bwana, mimi ni mwanaob na ninaongozwa na Roho mtakatifu, Sina kitu cha kuogopa. Roho Mtakatifu anaungana na roho yangu kuthibitisha kwamba mimi ni mwana wako.

Baba, wewe uko usukani na uatawala kila kitu. Sina chochote cha kuogopa kwani wewe ni Abba, baba

Ahsante, Bwana Mungu. Naomba uendelee kunibariki kwa amani yako. Na Baba., ninawaombea wengine ambao vilevile wahitaji rehema yako na neema katika kushinda woga. Baba, ninaomba kwa jina kuu la Yesu. Amina

Maombi ya Kurejelea (Methali 18:10, Waraka wa Kwanza wa Yohana 4:4, Warumi 8: 14-16)

<u>Maombi kwa Ajili ya Imani na Matumaini Katika Mungu</u>

Bwana, naja kwako na makusudio ya maombi yangu. Ninajua kwamba unasikia maombi yangu. Bwana , kuna wakati ninakua mdhaifu na nina shaka kwenye nia zangu. Kuna wakati imani yangu ni dhaifu. Naomba unisamehe kwa nyakati hizo ambazo imani yangu inakuwa dhaifu. Nisamehe kwa kutoamini.

Imani huja kwa kusikia neno la Mungu. Naomba unibariki ili nitumie muda mwingi nikisoma bibilia, ambayo ni neno lako takatifu. Tafadhali zidisha imani yangu. Imani ni ule ujasiri tulio nao kwamba lile tulitarajialo litatendeka. Inatuhakikishia yale mambo tusiyoyaona. Naomba unibariki ili imani yangu ndani yako izidi.

Ninajua kwamba wewe ni Mungu wetu utupendaye na ambaye hujibu maombi yetu. Iwapo kile ninachoombea si kizuri, tafadhali unibariki na kile kilicho bora zaidi kwangu. Bwana mtakatifu, umeahidi kwamba una mipango mikubwa kwa ajili yangu na maisha yangu, mipango ya amani, kunipatia siku za usoni zinazong'aa na matumaini. Ninaamini kwamba mpango ulionao kwa ajili yangu ndio mpango bora zaidi. Nifundishe kuwa mtiifu kwako. Wewe ni Mungu wa matumaini. Naomba unijaze kikamilifu kwa furaha na amani kwa maana ninakutumaini. Ndipo nitabubujika na ujasiri wa matumaini kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

Ninaomba vilevile kwa ajili ya watu wengine amao huenda wanang'ang'ana na imani yao na wanahitaji kuwa na ujuzi wa nuru ya matumaini, ambayo ni wewe, Bwana.

Baba, katika jina la Yesu Krristo, nimeomba. Amina.

Maandiko ya Kurejelea (Warumi 10:17, Yeremia 29:11, Warumi 15:13, Waebrania 11:1)

Maombi ya Upendo – Kushinda Uovu kwa Upendo wa Yesu

Baba wetu wa mbinguni mwenye upendo, twaleta kwako kwa maombi, wale watu ambao wamejaribu kutenda maovu katika familia zetu na wamejaribu kutuumiza wakijua au kwa kutokujua. Baba, umetuagiza tuwasamehe wengine. Kwa hivyo, tunasamehe kila mmoja wa watu hawa na tunaomba amani na ufanisi wa watu hawa. Wabariki na neema yako, amani na rehema.

Bwana Yesu, Umesema kwamba – Lakini ninawaambieni, mkapende adui zenu, mkabariki wale wanaowalaani, tendeni wema kwa wao wanaowachukia na waombeeni wale wanaowatumia vibaya na kuwatesa, ili muweze kuwa wana wa baba yenu wa mbinguni; kwa maana yeye huwaangazia jua wale waovu na hata wema, na anatuma mvua kwa wenye haki na wasiokuwa na haki.

Bwana, tunakutii wewe. Na tunaomba kwa ajili ya watu hawa wote ili uwabariki kwa upendo wako, amani na furaha. Acha wakujue wewe na wawe na ujuzi wako kwa njia ya kipekee. Baba, ninaomba kwa jina kuu la Yesu, Amina.

Maandiko ya Kurejelea (Mathayo 5: 44-45)

Maombi ya Kujisalimisha – Kumruhusu Mungu Kutawala Maisha Yangu

Bwana , umesema “ Ombeni, nanyi mtapewa, tafuteni, na mtapata; bisheni na mtafunguliwa”. Niko hapa, Bwana. Ninauliza ukaingie maishani mwangu. Ninatafuta mapenzi yako, Bwana. Ninasalimisha maisha yangu kwako. Bwana, ninakupa nafasi ya kwanza maishani mwangu. Naomba uchukue usukani na utawale maisha yangu kwa maana ninajua mpango wako kwangu ndio mpango bora zaidi.

Ninajua kwamba wewe ni Mungu wetu utupendaye na ambaye hujibu maombi yetu. Iwapo kile ninachoombea si kizuri, tafadhali unibariki na kile kilicho bora zaidi kwangu. Bwana mtakatifu, umeahidi kwamba una mipango mikubwa kwa ajili yangu na maisha yangu, mipango ya amani, kunipatia siku za usoni zinazong’aa na matumaini. Ninaamini kwamba mpango ulionao kwa ajili yangu ndio mpango bora zaidi. Jinsi mbingu zilivyo mbali na ardhi, ndivyo mawazo na mipango yako ilivyo juu zaidi ya mawazo yangu na mipango yangu. Nifundishe kukutii wewe. Acha ikawe kwangu kulingana na neno lako.

Nifundishe njia zako, ewe Bwana, ili nikaweze kuishi kulingana na ukweli wako! Nipatie usafi wa moyo, ili nikaweze kukuheshimu.

Baba, ninaomba katika jina kuu la Yesu. Amina

Maandiko ya Kurejelea (Mathayo 7:7, Zaburi 86:11, Yeremia 29:11, Luke 1:38, Isaya 55:9)